**Maelezo**: Katika maandiko hapo juu, amani hulinganishwa na ladha ya chumvi. Kama vile chumvi bila ladha yake ni bure, hivyo Injili bila amani ni bure na haiweze kufanya kazi, na huwa kama kumeza donge chungu.

8. Dunia itajuaje kwamba sisi ni watoto wa Elohim? Mathayo 5:9.

*******************************

**Somo La Tarehe 26 Desemba.**

## IMANI - HITAJI LA MAISHA YA UTAUWA

**Somo Kuu: 2 Wakorintho 4**
**Fungu La Kukariri: Waebrania 4:2**

1. Ili kumpendeza Elohim, tunafaa kumiliki nini? Waebrania 11:6.
2. Ni wapi ambapo kulikuwa na tendo la kwanza la imani katika upatanisho wa damu? Waebrania 11:4.
3. Ni kitendo gani cha imani kilihitajika jioni ya Pasaka? Kutoka 12:7.

**Maelezo**: Kuwaua kondoo wa Pasaka ilikuwa haitoshi. Ilibidi kila mmoja kujua kama damu imepakwa kwa miimo ya nyumba. Haitoshi leo kwa kujua kwamba Masihi aliishi na kufa, kwani kila mtu lazima ajitoe mwenyewe kwa dhabihu aliyoifanya kwa ajili yetu.



3. Je, ni maagizo yapi kuhusu maombi yametolewa kwa watu wa Elohim? Luka 21:36; 1 Wathesalonike 5:17; Wakolosai 4:2.
4. Kwa nini tunafaa kutia bidii katika maombi? 1 Petro 5:8.
5. Je, ni mfano gani wa Yahshua kuhusu maombi? Marko 1:35; Luka 22:44; Waebrania 5:7.
6. Yahshua alikuwa na hakika kwamba Elohim kwa wakati wote alisikia maombi yake? Yohana 11:41, 42.
7. Je, tunapaswa kuwa na uhakika kama huo? Mathayo 7:7, 8; Yakobo 5:17, 18.
8. Ni katika masharti gani Elohim ameahidi kusikia na kujibu maombi yetu? 1 Yohana 3:22; 5:14, 15
9. Je, ni nini kwa wakati mwingine huzuia maombi kukosa kujibiwa? Mithali 28: 9; Yakobo 1:6-8;4:3; Zaburi 66:18.
10. Ni faraja gani hutolewa kwa wale ambao huomba wakati wako katika shida? Zaburi 34: 7; 46: 1-3; 107: 6.
11. Maombi yetu kwa kweli hufika mbele za Elohim? Rev. 8:3; 5:8.
12 Ni mfano gani ambao tunapaswa kuepuka wakati kuomba? Mathayo 6:5-8.
13. Ni maagizo yapi yametolewa kwa masalio ya Kanisa? Ni matokeo gani yatafuatia kama tutafuata himizo hili? Wafilipi 4:5-7.

*******************************

**Somo La Tarehe 28 Oktoba.**

## UMUHIMU WA WALIMU



mfano bora tunapoweza na kuomba kila siku kupata roho kama ya Masihi.

8. Je, ni baadhi ya mambo yapi tunaambiwa tuyafuate ili tuwe mifano mizuri zaidi katika maisha yetu? Warumi 14:19, pia ona 1 Timotheo 6:11.

**Maelezo**: Nyakati nyingi sisi husahau kwamba twafaa kuwa mwanga wa dunia, na twafaa kufuata mifano tuliyoachiwa katika Neno la Elohim.

*******************************



***"Utakieni Yerusalemu amani; Na wafanikiwe wakupendao." Zaburi 122: 6***



# Masomo Ya Biblia

**kwa**
**KANISA LA ELOHIM (COG)**
**Siku Ya Saba (7th day)**

**Robo Ya Nne**
**2017**

**Ya**
**Oktoba, Novemba, Desemba.**
**Kutumiwa na Biblia**

**Watenda kazi wanahitajika, Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache...**

**Tuma maombi yote kwa S.L.P 568, Jerusalem - Israel**

**Somo Kuu: Tito 2**
**Fungu La Kukariri: 1 Petro 5:10.**

1. Je, bado tunahitaji walimu katika kazi ya kuwafanya Watakatifu kuwa wakamilifu? Waefeso4:11, 12.
2. Je, wahudumu wanafaa kuwa na uwezo wa kufundisha? 2 Timothy1:11.
3. Je, mtu anafaa kuwa na nini ili kuhitimu katika cheo cha askofu au mzee wa kanisa? 1 Timotheo 3:2.
4. Ni mfano gani wa ufundishaji bora tunapata katika Matendo ya Mitume 18: 24-28?
5. Ni tabia gani maalum inafanya mtu kuwa mwalimu bora? 2 Timotheo 2:24-26.
6. Ni nani ambaye alikuwa mwalimu mkuu? Mathayo 13:54.
7. Je, mwalimu wa kweli anafaa kuwa na uwezo wa kuwavutia na kuwahamasisha wasikilizaji wake? Luka 24:32; Mathayo 7:29.
8. Paulo alinena kuhusu watu fulani. Alisema walichokihitaji ni nini? Waebrania 5:12, 13. Aliashiria kwamba ukuaji ni muhimu?
9. Jinsi gani mtu atakuwa mwenye ujuzi katika neno? Waebrania 5:14.

**Maelezo**: Mafundisho ni moja ya Idara tano za huduma. Pia tazama katika mistari ya 8, 10 na 11 ya Efe 4, kwamba ni Bwana ambaye anasimamia kuhakikisha kwamba ofisi zote za huduma zimejazwa. Vipawa za mbinguni na miito zinapeanwa kwa madhumuni ya kuwasaidia wengine. 1 Wakorintho 12:31; 14:1, 12.



nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma. Nami utukufu ule ulionipa nimewapa wao; ili wawe na umoja kama sisi tulivyo umoja. . .Mimi ndani yao, nawe ndani yangu, ili wawe wamekamilika katika umoja "(Yohana 17:21-23). Ushahidi wa umoja wetu utasababisha dunia ijue kwamba Injili ambayo tunakiri ni ya kweli. Kwa upande mwingine, ikiwa watu wa Elohim watajulikana kwa ubishi na ugomvi, hii itakuwa onyesho mbaya juu ya Masihi. Tunapojifunza kile Biblia inasema juu ya somo hili muhimu, hebu tujitahidi kusafisha mioyo yetu kutokana na mawazo yote yenye utata na kuungana katika mapenzi kamili ya Elohim.

**Somo Kuu: 1 Wathesalonike 5: 9-15.**
**Fungu La Kukariri: 1 Wakorintho 11:16.**

1. Nini husababisha mapigano na ubishi? Yakobo 4: 1; Mithali 26:21; Mithali 22:10; Mithali 13:10.
2. Je, hata baadhi wanaokiri kuwa WaMasihi hupanda mbegu za fitina? Wafilipi 1:15-16.
3. Je, Biblia hukubali mijadala juu ya masuala madogo ya mafundisho? Tito 3:9.
4. Je, unapaswa kufanya nini wakati mtu mwingine hutoa changamoto kwa namna yenye utata? 1 Petro 3:8-11.
5. Nini tofauti kati ya mtu mwenye hekima machoni pa Elohim? Yakobo 3:13-18.
6. Nini tofauti kati ya mtu mpumbavu? Mithali 18:6-8.
7. Ni nini kinachofananishwa na amani? Marko 9:50.



**Somo La Tarehe 7 Oktoba.**

## KUVUMILIA MATESO

**Somo Kuu: 1 Petro 4**
**Fungu La Kukariri: 1 Petro 1:7**

1. Je, Mtume Petro anasema nini kuhusu mateso ambayo sisi kama WaMasihi tutayapata? 1 Petro 4:12.
2. Kwa nini WaMasihi hawafai kudhani ni jambo geni kuhusu mateso haya? 2 Timotheo 3:12; 1 Wathesalonike 3:3, 4.
3. Manabii wa kale walikuwa mifano ya waliopata mateso? Yakobo 5:10; Mathayo 5:12.
4. Ni katika njia gani wengi wao walijaribu? Waebrania 11:36-38.
5. Je, Masihi alisema nini kuhusu majaribu? Mathayo 5:10-12.
6. Kwa nini MMasihi anafaa kufurahi katika dhiki? Warumi 5:3-5.
7. Majaribu yana manufaa? 1 Petro 1:7; Yakobo 1:12.
8. Tumeahidiwa nini kama tunateseka kwa uvumilivu pamoja na Masihi? 2 Timotheo 2:12; Warumi 8:17.
9. Kama mtu atapata mateso kwa ajili ya kuwa MMasihi, huyo mtu anafaa kufurahi? Yakobo 5:11; 1 Petro 4:13.
10. Ni ahadi gani imewekwa kwa wale ambao watavumilia kwa uaminifu hadi mwisho? Mathayo 10:22; Ufunuo 2:10.
11. Mateso ya wakati huu yanaweza kulinganishwa na utukufu ule utakaofunuliwa? Warumi 8:18.



ataruhusu ndani ya hema lake? Zaburi 15:1-3.

********************************

**Somo La Tarehe 30 Desemba.**

## MFANO WA MMASIHI

**Somo Kuu: Wafilipi 4: 1-13.**
**Fungu La Kukariri: Wakolosai 3:12.**

1. Ni nani ni tunawakilisha na ni kwa namna gani? 1 Timotheo 4:12.
2. Ni nani ni tumeagizwa kufuata kama mfano wetu? Marko 8:34.
3. Ni kina nani tumetolewa kama mifano ya uvumilivu? Yakobo 5:10, pia ona 1 Petro 2:21.
4. Ni mtazamo gani dunia inafaa kuona katika sisi baada ya kuwekwa katika majaribu? 1 Petro 4:16.
5. Ni nini nia zetu zafaa kutafakari ili kutufanya mifano bora? Wafilipi 4:8.
6. Ni kwa njia gani tunapaswa kuwasiliana mmoja kwa mwingine? Waefeso 4:29.
7. Tufaa kujivika nini? Wakolosai 3:12.

Kwa mfano wetu wa maisha ya umasihi tutaweza kuvuta nafsi nyingi kwa Ufalme. Kwa hivyo ni muhimu sana kuwa

8. Wakati tunapojazwa na Roho, jinsi gani tutakavyoenenda? Wagalatia 5:16, 25, 26; Warumi 6:11-13.
9. Tunda gani la utakatifu litadhihirika wazi katika maisha yetu ikiwa tutajisalimisha kwa Mwokozi kabisa? Waefeso 5:9, 10; Wagalatia 5:22, 23.

**Maelezo**: Wengi leo hawajakubali kujitolea kwa Bwana kabisa na hawana furaha iliyo yakuwatosheleza kwa kina katika maisha yao ya uMasihi. Kumtumikia Masihi, kwao, ni mzigo badala ya furaha. Kama wewe haujajitolea kwa yote kwake Bwana— fanya hivyo leo!

********************************

**Somo La Tarehe 9 Desemba.**

## UBISHI - ZANA YA SHETANI

"Nyumba ambayo imegawanyika makundimakundi yanayopingana haiwezi kudumu," Masihi alisema. Huu ni ukweli maalumu hasa unaotumika kwa Kanisa leo. Ugomvi na mgawanyiko umejaa kila mahali na ni zana ambazo Shetani anatumia kufanya watu wa Elohim wawe wadhaifu. Biblia inafundisha kwa ushupavu dhidi ya ugomvi na ubishi kati ya ndugu. Masihi huangalia watu ambao hufuata mfano wake katika upendo wa kindugu. Masihi alijihusisha sana kuhusu jambo hili katika maombi yake kwa wafuasi wake. Hamu yake kuu ni kwamba, "Wote wawe na umoja kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao



10. Ni maneno gani mazuri Yakobo aliandika kuhusu kupeanwa kwa zawadi? Yakobo 1:17.

********************************

**Somo La Tarehe 4 Novemba.**

## USAWA KATIKA WOKOVU

**Somo Kuu: Warumi 9:1-8; Yohana 8:30-44.**
**Fungu La Kukariri: Wagalatia 3:28.**

1., Baba yetu wa Mbinguni ana mapendeleo ya watu? 1 Petro 1:17-19.
2. Ni wana wa Ibrahimu wote wataokolewa? Warumi 9:8.
3. Ni kupitia nani na ni jinsi gani watoto wa ufalme wanaitwa? Warumi 9:7 (sehemu ya mwisho); Wagalatia 3:16.
4. Jinsi gani tutakuwa warithi wa ahadi zilizofanywa kwa Ibrahimu, na hivyo kupokea uzima wa milele? Wagalatia 3:29.
5. Ni wote wa uzao wa Ibrahimu kupitia Yakobo wataokolewa, au itakuwa mabaki tu? Warumi 11:5; Isaya 10:21, 22.
6. Kama vile wanavyoendelea kukusanywa kurudi nchi ya ahadi, Yerusalemu, na nchi jirani, watatumiwa wachungaji kuwafundisha ukweli? Yeremia 3:14, 15; Ezekieli 33: 6-8, 20.



"mgeni" – ni kwa sababu hii yeye uanza kusingizia! Kwa hakika, baadhi ya nia kuu za kusingizia ni hisia za kujiona duni na wivu, ambao uletwa juu ya hali dhaifu ya kiroho na haja ya kuhalalisha mtu binafsi kwa kusingizia wengine.

**Somo Kuu: Waefeso sura ya 4.**
**Fungu La Kukariri: Waefeso 4:29.**

1. Ni nini chanzo cha kusingizia? Mathayo 15:19; Luka 6:45.
2. Je, tunafaa kuwaamini wale ambao ujiingiza katika kusingizia? Yeremia 9:8.
3. Nini kundi lipi la watu hufurahia kusengenya? Mithali 11: 9; Zaburi 50:20; Yeremia 6:28.
4. Ni athari gani za kusingizia? Mithali 6:19.16: 28, 18: 8, 26:20.
5. Mwisho wa umbeya unaoudhi, maongezi yenye ladha, maneno yaliyotiwa chumvi na uvumi ni nini? Mhubiri 10:12-14.
6. Je, sisi tutahalalishwa tukiongea maneno mabaya kwa watu fulani ambao tunadhani wanastahili hayo maneno? Tito 3:2-8.
7. Je, tutahitajika kutoa hesabu ya maneno yetu yote ambayo si ya kweli na yenye kudhuru? Mathayo 12:36,37.
8. Je, watu wanaonekana wachaji Elohim, wakati mwingine uanguka katika dhambi ya kusingizia na kuzungumza mabaya? Yakobo 1:26.
9. Ni kuhitimu kupi kunaohitajika kwa wale ambao Bwana



**Maelezo**: Kwa mujibu wa maandiko, mateso makali yalikuwapo ambayo WaMasihi kwa wakati wote wamepitia kutoka kwa maadui wa Masihi, na itakuwa hivyo hadi kurudi kwa Bwana na Mwokozi wetu.

********************************

**Somo La Tarehe 14 Oktoba.**

## USILITAJE JINA LAKE BURE

**Somo Kuu: Waefeso 5:1-20**
**Fungu La Kukariri: Kutoka 20:7**

1. Yahshua alisema nini kuhusu kuapa? Mathayo 5:33-37.
2. Jinsi gani Yakobo anatuelekeza kufanya wakati tunaambiwa tuape? Yakobo 5:12.
3. Kama mtu yeyote aliapa kwa uongo wakati wa Walawi, jinsi gani aliadhibiwa? Mambo ya Walawi 6:2-6.

**Maelezo**: Tunaona kwamba kuapa hakukukatazwa katika sheria ya Musa. Hata hivyo Yahshua alikuja ili kuitukuza sheria (Isaya 42:21) na hii inakataza kuapa.

4. Jinsi gani ni kosa kulitaja jina la Bwana Elohim wetu bure? Mambo ya Walawi 24:11-14.
5. Paulo alisema nini kuhusu kusema maneno yasiyo na maana? Waefeso 5:4, 6; 4:29; Wakolosai 3:8.

7. Tunaambiwa nini kuhusu mioyo ya wachungaji hawa? Yeremia 3:15.
8. Je, wachungaji, anaowapeleka Bwana kwa Israeli wakati wanapokusanywa, watafanikiwa katika kuwafundisha ili wengi wapokee moyo mpya na roho mpya? Ezekieli 36:24-26.

**Maelezo**: Ni vizuri kukumbuka kwamba watu, waliojawa na Roho Mtakatifu, walienda kwa Mataifa, kuhubiri injili, na mioyo ya mamilioni imebadilishwa kutoka kwa ibada ya sanamu na kumtumikia na kumwabudu Bwana. Kazi yake Bwana ni sawa leo kwa Israeli. Kazi hii inaendelea mbele kupitia Biblia, neno la Elohim, pia na Roho wake ndani ya watumishi wateule, aliowachagua — bila mapendeleo kwa mtu, taifa au rangi. Rev. 22:16, 17

8. Katika siku ile Bwana atawatakasa wengi katika nyoyo zao na kuweka ndani yao Roho wake, nini imesemwa kuhusu kujenga miji iliyo ukiwa na kuweka kuta? Ezekieli 36:33-35.
9. Matukio ya baadaye yahusuyo Israeli yatakuwa na athari gani katika kufungua macho ya watu wa mataifa yote? Ezekieli 38: 14-16, 23.

**Maelezo**: Hii haimaanishi kwamba watu wa mataifa, wataokolewa tena kuliko jinsi ile Wayahudi wanavyookelewa, kwa sababu tu walifanywa kutambua kuna Elohim atawalaye ulimwengu bado. Kutakuwa na ujumbe wa onyo kwa wote, kwa mataifa yote, kazi ya neema iliyo kamilika, kabla ya kilele kuja. Warumi 11:12.



11. Ni nini kitakachotokea kutokana na kukua katika neema? 2 Petro 1:8.
12. Ikiwa tutashindwa katika mambo haya, ni nini tutakuwa tumesahau? 2 Petro 1:9.

*******************************

**Somo La Tarehe 2 Desemba.**

## MAJI YA UZIMA

**Somo Kuu: Isaya 12**
**Fungu La Kukariri: Ufunuo 22:17.**

1. Mwaliko wa Elohim kwa wote wenye kiu ni upi? Isaya 44: 3; 55: 1.
2. Ni kwa njia gani tutateka maji kutoka visima vya wokovu? Isaya 12: 2, 3.
3. Ni ombi lipi rahisi Yahshua alifanya kwa yule mwanamke katika kisima cha Yakobo? Yohana 4: 6, 7.
4. Jibu lake mwanamke lilikuwa lipi? Yohana 4:9.
5. Jinsi gani mwanamke alijibu wakati Yahshua alimwambia kuhusu maji ya uzima? Yohana 4:10-12.
6. Wakati mtu anapokea 'Maji ya uzima', mahitaji yake ya ndani yatakuwa yametimilizwa? Yohana 4:13, 14; 6: 35.
7. Katika tukio tofauti mwaliko gani uliweza kumfikia kila mmoja wetu, na ni jinsi gani Yahshua alieleza kuhusu maji haya ya kiroho ya uhai? Yohana 7:37-39.



6. Bwana ametuahidia nini kama tutaelekeza mazungumzo yetu kuwa mema? Zaburi 50: 23.
7. Tutaweza kuelekeza mazungumzo yetu kuwa mema bila ya mabadiliko ya moyo? Mathayo 12:34, 35.
8. Tutahukumiwa kwa yale yote tutakayonena? Mathayo 12:36, 37.
9. Ni nini Yakobo alisema kuhusu ulimi? Yakobo 3:6-10.
10. Ni kwa njia gani mbingu itatuangalia tukishindwa kumtumikia Elohim kwa mioyo yetu yote na kuweka kando amri zake takatifu ili kufuata mapokeo ya wanadamu? Marko 7:7-9.
11. Tutapatikana bila hatia kama tutalitumia jina la Bwana bure kwa njia yoyote? Kutoka 20:7.

**Maelezo**: Tumehakikishiwa katika maandiko matakatifu ya Elohim kwamba hatutakosa kupatikana na hatia kama tutalitumia jina la Bwana bure, kama vile katika kuapishwa, au katika kuchukua kiapo, au kama tutakataa kutunza amri za Elohim, na kufuata desturi za watu badala yake.

*******************************

**Somo La Tarehe 14 Oktoba.**

## NI LAZIMA MTU AZALIWE TENA

**Somo Kuu: Waefeso 3**
**Fungu La Kukariri: Yohana 3:3**



**Maelezo**: Biblia inatuambia "kesheni na kuomba". Mafanikio makubwa yanaweza kupatikana kwa maombi ya watu wake. Hebu tuendelee kuomba, kama vile Biblia imetuamrisha, kwa ajili ya amani ya Yerusalemu, kwa ajili ya viongozi wa mataifa yetu na kwa ajili ya ndugu zetu na dada duniani kote.

*******************************

**Somo La Tarehe 23 Desemba.**

## KUSINGIZIA NA KUONGEA UOVU

Hakuna mtu anapenda kusengenywa, wala hakuna mtu yeyote hufurahia kusingiziwa. Hata hivyo ni hakika hakuna uhaba wa wambeya au wasingiziaji. Hii inaonyesha kwamba wengi hawana chuki halisi kwa ajili ya michezo yenyewe, na kwamba ni wakati tu wao wenyewe huwa malengo ya mishale yake ya uchungu wao ufahamu kikamilifu unyarafu wake. Wakati mwingine tunajikuta tukishiriki katika aina yoyote ya "kuzungumza mabaya" au uvumi usio na huruma, tunafaa kufanya vizuri kuchunguza nia zetu. Tungefaa pia kufanya vizuri tujiulize kama sisi kweli tunajua nini tunazungumzia. Mara nyingi watu hurudia mambo ambayo hawana ukweli dhabiti. Wanaweza hata kutojua mtu ambaye wanasingizia, lakini wamesikia tu "hili na lile" kutoka kwa baadhi ya "mwandani wake." Mwandani huyu mara nyingi, katika hali halisi, ni

12. Tutaweza kubeba msalaba kwa furaha, na kujikana wenyewe katika kazi ya Bwana? Luka 9:23-25.
.

*******************************

**Somo La Tarehe 25 Novemba.**

## KUKUA KATIKA NEEMA

**Somo Kuu: Waefeso 4**
**Fungu La Kukariri: Wagalatia 2:20.**

1. Lengo letu kuu kama WaMasihi ni lipi? 2 Yohana 3:2, 3.
2. Ili kuona Elohim ni nini lazima tumiliki? Waebrania 12:14.
3. Katika kuvaa utu upya jinsi gani tutakuwa? Waefeso 4:24.
4. Ushuhuda wetu kwa ulimwengu ni upi? Wagalatia 2:20.
5. Ni kupitia hatua zipi tutaweza kukua? 2 Petro 1:5-7.
6. Jinsi gani imani ni muhimu kwa MMasihi? Waebrania 11:6.
7. Je, mwito wetu mkuu ni upi? 2 Petro 1:3; Wafilipi 3:14.
8. Tukiisha kupata imani na wema, ni nini lazima tuwe na bidii kutafuta? 2 Petro 1:5; Wakolosai 2:2, 3.
9. Maarifa yatatuongoza kwa? 2 Petro 1:6; 1wakorintho 9:24-27.
10. Ni nini itafuatia ikiwa tutafikia kiwango cha uMasihi? Yohana 17:21-23.



10. Kwa nini Wayahudi walikatiliwa mbali, na ni wakati gani upofu huu utaondolewa kutoka kwao? Warumi 11:20-25.

*******************************

**Somo La Tarehe 11 Novemba.**

## IBADA NA KUTAKASWA

**Somo Kuu: 1 Petro 1**
**Fungu La Kukariri; 1 Petro 2:23.**

1. Je, Elohim anatarajia watu wake kujitolea katika huduma yake katika wakati huu? Warumi 12:1.
2. Bwana alitoa amri kwa Walawi kwa Hezekia? Amri hii ilikuwa ipi? 2 Mambo ya Nyakati 29: 5-11.
3. Mtazamo wao kwa huu wito wa huduma ulikuwa upi? 2 Mambo ya Nyakati 29: 15-19.
4. Walawi walifanya utakaso wowote kwa Elohim? 2 Mambo ya Nyakati 29:30-32.
5. Maombi yao yaliathirika kutokana na utakaso huo? 2 Mambo ya Nyakati 30: 26, 27.
6. Ni katika njia ipi tunapaswa kumtukuza Baba yetu wa Mbinguni? 1 Wakorintho 6:20.
7. Ni ahadi gani Bwana alisema kwamba itaingia na kukaa ndani yetu, baada ya miili yetu kutakaswa na kuwa huru kutokana na dhambi? 2 Wakorintho 6:19.



12. Ni nani tu atapokea hitaji kamili la Elohim? Ufunuo 14:12.

*******************************

**Somo La Tarehe 23 Desemba.**

## OMBA BILA KUKOMA

**Somo Kuu: Zaburi 66:13-20.**
**Fungu La Kukariri: Zaburi 6:9**

1. Bwana husikia maombi ya watu wake? Mithali 15:29.
2. Je, Yeye atasikia maombi yetu wakati tunajua na kubaki katika kutotii? Mithali 28: 9.
3. Tutapata nini kupitia maombi? Mathayo 21:22.
4. Je, Masihi anasema nini kuhusu maombi ya unafiki? Mathayo 23:14.
5. Ni mifano gani mizuri tumepewa kufuata katika Matendo 1:14 na 6:4?
6. Ni mara ngapi tutaenda mbele za Bwana katika sala? Waefeso 6:18; Soma pia Warumi 12:12 na Wakolosai 4:2.
7. Tunapaswa kufanya nini ikiwa ndugu au dada anapitia majaribu? Matendo ya Mitume 12:5.
8. Jinsi gani kuna umuhimu katika sala ya imani? Yakobo 5:15.
9. Jinsi gani tutaweza kila siku kujenga, kuinuana, na kusaidiana katika mahitaji ya kila mmoja? Yakobo 5:16.



1. Ni nini nabii Malaki alisema kuhusu mjumbe ambaye atatangaza Bwana? Bwana Yahshua angefanya nini wakati angelikuja? Malaki 3:1-3.
2. Ni nini Isaya alitabiri kuhusu huyu mmoja aliyechaguliwa kuandaa njia kwa ajili ya Mkombozi wa dunia aliyengojewa kwa muda mrefu? Isaya 40: 3.
3. Wakati Mjumbe huyu ambaye manabii walizungumza kumhusu angelikuja, uzito wa ujumbe wake ungekuwa upi? Mathayo 3:1-3.

**Maelezo**: Watu waliokuja kwa Yohana Mbatizaji wakitamani kubatizwa, si kwamba walikubali ukweli tu, lakini pia walikuwa na huzuni kwa sababu ya dhambi zao na walitubu na kuikiri kwa Elohim. Wale waliokataa kutubu dhambi zao za zamani walikuwa wanarudishwa.

4. Yohana Mbatizaji alisema nini kuhusu Yahshua, ambaye alikuwa akitayarisha njia yake? Mathayo 3:10-12.
5. Muda mfupi baada ya Yahshua kuanza huduma yake, ni nani ambaye alikuja kwake? Alisema nini? Yohana 3:1, 2.

**Maelezo**: Inawezekana kwamba Nikodemo aliona aibu kuonekana na Yahshua, na kwa hivyo alichagua kuja usiku, wakati hatari ya kuonekana na marafiki zake wasioamini ingekuwa dogo? Hii inalingana na watu katika siku hii na wakati huu ambao wamesikia kuhusu Bwana, lakini wanaogopa kukiri kwake, katika uwepo wa marafiki zao wa kidunia.

8. Je, Paulo anasema nini kuhusu mwili wake? Wafilipi 1:20.
9. Utakaso wa Yahshua Masihi ulimwongoza kufanya nini? Wafilipi 2:5-8.
10. Ni nini lazima kila mmoja ambaye ni wa Masihi anafaa kumiliki? Warumi 8:9.
11. Wakati tumetakaswa kikamilifu, tutaweza kuitikia wito? Isaya 6:8.
12. Maisha ya Masihi yalikuwa moja ya huduma? Mathayo 20:27, 28; Luka 22:27.
13. Jinsi gani utakaso na kuwekwa wakfu inakamilishwa? Warumi 15:16; Yohana 17:17, 18.
14. Je, ni kuwa kamili? 1 Wathesalonike 5:23.

*******************************

**Somo La Tarehe 18 Novemba.**

## KUNUNG'UNIKA

**Somo Kuu: 1 Wakorintho 10:1-11**
**Fungu La Kukariri: Wafilipi 2:14, 15.**

1. Baada ya Elohim kuwakoa kwa njia ya ajabu wana wa Israeli kutoka kwa Wamisri na kuwaleta kupitia Bahari ya Shamu, walifanya nini? Hesabu 14:2-4.
2. Waliweza kuridhika na kile Elohim aliwapatia kula? Hesabu 11:4-6.
3. Elohim alifurahishwa na kunung'unika kwao? Jinsi gani Yeye aliwadhibu? Hesabu 11:1.



4. Ni adhabu gani zaidi ya kutisha ililetwa juu ya wana wa Israeli kwa sababu ya dhambi hii? Hesabu 14:26-30.
5. Ni wanaume wangapi wa wana wa Israeli waliotoka nchi ya Misri? Kutoka 12:37.

**Maelezo**: Kulikuwa na watu elfu mia sita ya watu wa Israeli walipotoka nchi yaMisri. Katika idadi hii kubwa ni watu wawili tu waliokuwa juu ya umri wa miaka 20 waliruhusiwa kuingia nchi ya ahadi. Wale wengine wote walikufia jangwani. Hivyo basi tunaona adhabu ya kutisha waliyoipokea.

6. Ni haki kwa watu kulalamika kuhusu hali ya maisha leo? 1 Wakorintho 10:10.
7. Wakati akizungumza kuhusu Israeli, kitu gani muhimu Paulo analeta katika akili zetu? 1 Wakorintho 10:6, 11.
8. Ni maagizo gani zaidi, Paulo anatoa kwetu na ni kwa nini? Wafilipi 2:14, 15.

**Maelezo**: Kulalamika (kunung'unika) hakuna nafasi katika maisha ya MMasihi. Tunaishi hili kutoa sifa kwa Muumba wetu. Sifa ni kinyume cha kunung'unika.

9. Ni nini haifai kamwe kupatikana katika mazungumzo yetu, ni nini lazima iwe hali ya maisha yetu ya kila siku kwa nyakati zote? Waebrania 13:5; 1 Timotheo 6:6-8.
10. Kama tunaye Bwana awe mwongozo wetu, ni nini itakuwa hali ya mioyo yetu? Zaburi 16:6, 9.
11. Je, ni aina gani ya habari tutakuwa tunapitisha kwa wengine? Isaya 52: 7.



6. Jinsi gani Yahshua alijibu Nikodemo? Yohana 3:3.
7. Wakati Nikodemo hakuelewa kuhusu kuzaliwa upya na kusema "Jinsi gani mambo haya yanawezekana?" Yahshua alimjibu vipi? Yohana 3:10-12.
8. Jinsi gani Yahshua alionyesha kwamba kuna umuhimu kwa mtu kuzaliwa upya? Yohana 3:5-8.
9. Ni nini ingine maandiko matakatifu ya Elohim yanasema kuhusu kuzaliwa upya? Yohana 1:12, 13; 1 Petro 1:23.
10. Ni kwa sababu gani mwana wa Elohim alidhihirishwa? 1 Yohana 3:5-9.

**Maelezo**: Utakaso (Masihi ndani yetu) na kubakia katika kweli kutokana na mateso na majaribio, ni njia yetu ya pekee yenye usalama, uhakika na nguvu.

11. Katika unabii wa Danieli wa mwisho wa wakati huu, ni makundi gani mawili ya watu yametajwa? Danieli 12:10.

*******************************

**Somo La Tarehe 21 Oktoba.**

## MAOMBI

**Somo Kuu: Mathayo 6:1-21**
**Fungu La Kukariri: 1 Wathesalonike 5:17.**

1. Jinsi gani mtunzi wa Zaburi alivyomwiita Muumba? Zaburi 65: 2.
2. Je, maombi ni nini? Zaburi 142:1.



4. Katika siku zilizopita, kwa nini neno halikuwa na faida kwa wana wa Israeli? Waebrania 4:2.
5. Jinsi gani Mwisraeli alionyesha imani katika upatanisho kwa umwagaji wa damu? Mambo ya Walawi 4:27-30.
6. Maelezo yaliyotolewa katika Biblia, imani ni nini? Waebrania 11:1
7. Ni wangapi wanayoimiliki imani hii? Warumi 12:3.
8. Jinsi gani wengi hujidai, ambayo inaonyesha ukosefu wa imani ndani yao? Yohana 6:30.
9. Kabla ya kuuona utukufu wa Elohim, tunapaswa kufanya nini? Yohana 11:40.

**Maelezo**: Yahshua angeweza kusema neno na jiwe lingeondoka chini ya udhibiti wa Elohim, lakini alichagua kutumia nguvu za kibinadamu kama inavyowezekana. Kwa ombi lake katika Yohana 11:39, ilionekana ukosefu wa imani katika moyo wa Martha. Baada ya nguvu za kibinadamu kufika kikomo chake, katika Yohana 11:41, Alitoa wito kwa Baba wa kufanya kile uwezo wa binadamu haukuweza kufanya; kufufua maiti. Tukiongea kwa kiroho, Elohim pekee yake anaweza kutufufua kutoka wafu na uozo wa kiroho.

10. Kwa nini Yahshua alimpongeza huyo ofisa kupita wengine? Mathayo. 8:5-8.
11. Ni nini hutuongoza kuamini kwamba Masihi atarudi hivi karibuni? Luka 18:8.